

**MUHULA WA PILI**  
**102/1**  
**KISWAHILI**  
**KIDATO CHA NNE**  
**KARATASI YA 1**  
**INSHA**  
**MUDA: SAA 1¾**  
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**1. Hii ni insha ya mahojiano. Ichukue mtindo wa tamthilia.**

kumb: mwanahabari ndiye anayehoji.

Baadhi ya hoja ni kama vile:

- (i) Kuleta vijana pamoja duniani na hivyo kupunguza tuhuma zinazoelekea kuleta vurugu kutokana na vijana kutofahamiana
- (ii) Usambazaji wa teknolojia inayorahisisha maisha ya vijana kote duniani kupitia kwa huduma zinazotolewa na simu.
- (iii) Kuendeleza biashara - kubadilishana bidhaa na pesa kupitia mtandao kama vile MPESA.
- (iv) Hurahisisha huduma za benki. Vijana wanaweza kufikia akaunti zao kupitia kwenye rununu.
- (v) Huwa na vifaa kama vile vikokotoo vya kurahisisha kufanya hesabu.
- (vi) Ni chombo cha burudani - vijana hupata michezo mbalimbali.
- (vii) Huimarisha utafiti. Vijana wanaweza kufanya utafiti kupitia kwenye rununu.
- (viii) Huweza kutumiwa kupigia picha, hivyo kuokoa pesa ambazo zingenunulia kamera au video.
- (ix) Vijana wanaweza kuwasiliana na familia zao kutoka mbali, hivyo kuokoa muda na fedha ambazo wangetumia kusafiri.
- (x) Vijana wanaweza kuhifadhi msahafu (Biblia au Korani) kwenye simu, hivyo kujikuza kiroho kila mara.
- (xi) Ni njia ya kupata habari kutoka kwenye mashirika ya usambazaji wa habari. Baadhi ya rununu zina redio na hata runinga. Vijana wanaweza kusikiliza na kutazama habari hata wakiwa safarini.
- (xii) Hufanikisha kuwanasa matapeli na magaidi wanaowadhuru vijana. Baadhi ya rununu huonyesha simu ilipopigiwa hivyo kusaidia kudhibiti mitandao ya uhalifu.

**2. Hii ni insha ya ufafanuzi. Mwnafunzi asipinge swali.**

Hoja ni kama vile:

- i. kudumisha umoja na upendo wa wananchi
- ii. kuwezesha wananchi kuendeleza biashara zao hivyo kujipatia mapato na kukuza uchumi wa taifa.
- iii. kuwawezesha wanasisa kuuza sera zao bila kutatizika
- iv. kuhakikisha usalama wa wananchi
- v. kuendeleza uzalendo kwa kutii sheria na katiba
- vi. kuwavutia wawekezaji wa kigeni
- vii. kuzuia uharibifu wa mali
- viii. kuwezesha masomo kuendelea shuleni
- ix. kuwezesha usafirishaji na usambazaji wa bidhaa

### **3. Mchuma janga hula na wa kwao**

Hii ni insha ya methali

Chuma ni kufanya kazi na kupata faida/ tungua matunda kutoka mtini.

Janga-balaa /baa / shida / hatari / taabu

Ajitafutiaye shida huathirika na jamii / jamaa yake .

Mtahiniwa asimulie kisa /visa vitakavyoafikiana na methali.

Asipinge methali.

Ruwaza zifuatazo zinaweza kujitokeza;

- Mhusika kushiriki raha za kilimwengu, akaambukizwa magonjwa yasiyotibika,hatimaye anarejea nyumbani anakougua , mzigo wa kumtunza unakuwa kwa familia yake.
- Mhusika aliyekuwa akifanya kazi katika kampuni au shirika fulani, Anafutwa kazi labda kutokana na uzembe au utovu wa maadili ya kikazi,anarejea nyumbani kwa familia yake; kule hana chochote hivyo basi anaishia kutegemea jamma zake, huu unakuwa mzigo mkubwa kwa watu wake.
- Mtoto ambaye anatokea kuwa mhalifu, anafikishwa kortini na kutozwa faini kubwa.Hii inakuwa gharama kwa familia yake kwa vile ndio wanaotakiwa kulipia.
- Mwanafunzi ambaye anakosa kuwajibika masomoni shuleni , anafeli mtihani, maisha ya halafu yanakuwa magumu kwa hivyo jamaa zake wanalazimika kuingilia kati ili kumuauni kwa mahitaji ya kila siku
- na kadhalika

### **4. Ni insha ya kubuni fikra**

Azingatie sehemu zote kv utangulizi, mwili, hitimisho.

Mtahiniwa atunge kisa kinachomalizia kifungu kilichotolewa.